

## **MUHULA WA TATU 2026**

### **MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA PILI KIDATO CHA TATU 102/2**

#### **1. Ufahamu**

- a. **Sababu ya kauli uongozo hutoka kwa Maulana kuonekana kinaya ya kupingwa na watu wengi.**  
Viongozi wengi wamekuwa katili ambapo wengi wao hutekeleza maovu bila kujali wala kubali. 1x1
- b. **Kiini cha watu wengi kuchukia viongozi wanaojisifu kila wakati.**
  - i). Viongozi kama hawa huwachosha na hata kuwachusha wafuasi wao.
  - ii). Huwafanya raia wajute kuwachagua. 1x2
- c. **Kueleza matokeo ya kiongozi kuwasaidia wanaotatizika maishani.**  
Watu huwa na imani naye. 1x1
- d. **Kutaja misingi mitatu inayotumiwa na baadhi ya viongozi kuwabagua wananchi.**
  - i). Misingi ya Kitabaka
  - ii) Misingi ya kijinsia
  - iii) Misingi ya kikabila
  - iv) Misingi ya kidini. 1x3
- e. **Maoni ya mwandishi kuhusu dhima ya mwananchi kuhakikisha kuwa uongozi bora umedumishwa.**  
Wananchi wana wajibu wa kuwachagua viongozi wanaofaa bila kupofushwa na ahadi zao za uongo. 1x1
- f. **Kutaja vitambulishi vinne vya viongozi bora.**
  - i) Mnyenyekevu
  - ii) Mwenye maadili
  - iii) Anayetetea haki za wanyonge
  - iv) Mpenda amani
  - v) Anayayejitenga na ubaguzi/ anayechunga maslahi ya watu wote.
  - vi) Mwajibikaji
  - vii) Mwenye huruma **( nne za kwanza)** 1x4
- g. **Kueleza maana ya maneno kama yalivyotumiwa katika ufahamu.**
  - i) mwongofu- mwadilifu/mwenye tabia nzuri
  - ii) kuwaauni - kuwasaidia.
  - iii) kite – huruma 1x3

#### **2. Ufupisho**

- a.
  - i) Vijana wana nafasi kubwa kukabiliana na maovu ya kijamii kwani ndio wengi.

- ii) Wanaweza kuwahamasisha wenzao dhidi ya tabia hasi.
- iii) Miradi ya vyama huwawezesha kutumia nishatu zao ili kujinufaisha na kuepuka maovu
- iv) Kushiriki vyama vya michezo humwezesha mwanafunzi kuimarisha afya na kujenga misuli.
- v) Kushiriki huku ni chanzo cha riziki baadaye.
- vi) Vyama vya wanafunzi ni msingi wa mshikamano namaridhiano. Visitumiwe kuwagawa wanafunzi kitabaka.
- vii) Mwanafunzi atenge muda wa shughuli za vyama na wa kudurusu masomo yake.

$$5 \times 1 = 5$$

$$\text{Mtiririko} = 1$$

$$\text{Jumla} = 6$$

- b. i). Mfumo waelimu unatilia mkazo mafunzo mengine ya nje ya masomo ya kawaida.
- ii). Vyama vya wanafunzi vinayapitisha mafunzo ya ziada.
- iii). Vyama hivi hutofautiana kulingana na majukumu.
- iv) Vyama hivi vina manufaa ya kuhusudiwa.
- v). Shuleni mwanafunzi anafunzwa kujiunga angaa na vyama viwili.
- vi) Hukuza kusaidia kukuza vipawa/ stadi ya kujieleza.
- vii). Huhimiza utangamano miongoni mwa wanachama kwa kujiona kama walio na mwelekeo mmoja.
- viii) Hujenga uhusiano wa kimataifa na kimataifa.
- ix) Huwawezesha wanafunzi kukabiliana na changamoto za maisha.
- x) Mwanafunzi hujifunza maadili ya kijamii na kidini.
- xi) Hujifunza kujistahi na kustahimili.
- xii) Majukumu anayopewa hupalilia uwajibikaji, uaminifu na uongozi .

$$8 \times 1 = 8 + 1 \text{ utiririko} = 9$$

#### **MATUMIZI YA LUGHA**

- a. kulinganisha /s/ na /z/ -Sauti za ufizi, vikwamizo.

kulinganua /s/ ni sikhuna /z/ ni ghuna.

kulinganisha /p/ na /b/ sauti za midomo, vipasho.

kulinganua /p/ sikhuna /b/ ghuna

$$1/2 \times 4$$

- b. Mwalimu

ua, oa, au

$$1 \times 2$$

- c. U-nafsi

-ta – wakati

$$(1/2 \times 4)$$

adhib-mzizi

iw – kauli

- a- kiishio
- d. Wewe hujamaliza kulima shamba ambalo.  
lisingalikuwa langu nisingalifurahi. **(2X1)**
- e. Mwalimu huwafunza wanafunzi kwa ustadi mkubwa. **(2x1)**
- f. kuonyesha mshangao: Lo! Mwizi amemuua jirani.  
kuonyesha amri: Ondoka hapa!  
kuonyesha taarifa: Nilimtembelea jana.  
kuonyesha swali: Umemwona Daniel? **1x2**
- g. Mimi na wewe tunapenda kusoma sana. **1/2x6**
- h. Ji-Ma – jiguu, maguu, jifya –mafya.  
Ja-Ma – jani- majani  
Ji-Me – jino –meno  
o-Ma – shati – mashati **1x2**
- i. i. Kuonyesha matumizi ya neno geni/lugha tofauti.  
\*Principal wa shule hii anafanya kazi kwa bidii.  
ii. Kuonyesha kosa la sarufi.  
Kiutu \*yangu ilipotea  
iii. Kuonyesha kosa la hijai. \*Balabala hii inaelekea Mombasa.  
iv. Kuashiria maelezo/ufafanuzi uliotolewa chini baada ya maandishi makuu. Shibli  
ameonekana kijijini. \*Shibli ni mtoto wa simba.  
v. Kuonyesha tahadhari. \*Kirejeshi ‘o’ na kirejeshi ‘amba’ havitumiwi katika sentensi moja.  
**1x2**
- j. Komu ameshona nguo vizuri na kuiuza sokoni.  
Komu aliuza nguo sokoni baada ya kuishona. **2x1**
- k. kuliko –kihusishi cha kulinganisha  
halafu – kihusishi cha wakati **1x2**
- l. “Kila mwanafunzi anafaa kuwa na nidhamu.” Mwalimu mkuu alisema **1/2x4**
- m. Shairi ambalo limekaririwa – kiima

- linapendeza – kiarifu 1x2=2
- n. Angalisoma mapema – tegemezi
- angalifaulu vyema – tegemezi 1x2
- o. Msicheze! 1x2
- p. Gombe hilo lilinunuliwa mbali na jiji lile. 2x1
- q. Kupita kwa mwanafunzi huyo kulitokana na kusoma kwake kwa bidii. 2x1
- r. Sokoni –kielezi
- ni –kitenzi kishirikishi kipungufu. 1/2x2
- s. Chakula – mlo ,maakuli,posho
- Chakura –pekua ,chimbachimba,vuruga 2x1
- Kuku wanachakura mchanga wakitafuta chakula. 2x1
- t. Yule mzembe – kirai nomino  
na wanawe – kira kihusishi 1/2x2
- u. Uhai – uhaishaji /uhuishi
- Mbinafsi – kubinafsisha /ubinafsishaji 1/2x2
- v. Yote – bila kubakisha/kusaza
- Yoyote – bila kubagua/kuchagua 1/2x2

#### **4.ISIMU JAMII**

- a. Sajili ya hospitalini/hospitali/zahanati/kituo cha matibabu
- b. (i) Matumizi ya msamiati teule/maalum “homa ya matumbo”  
(ii)Utohozi lebu,daktari  
(iii)Kuchanganya ndimi “Ni acute”  
(iv)Matumizi ya lugha ya kitaaluma “penobarbital” “widal test”  
(v)Lugha ya tarakimu “Tembe za pentobarbital mbili mara tatu”  
(vi)Matumizi ya vifupisho “CD4” “VCT” “TB”  
(vii)Matumizi ya lugha sanifu “Ni hali...”  
(viii)Matumizi ya lugha ya kudadisi  
(ix)Matumizi ya lugha ya upole “utapona haraka”  
(x)Kutaja vyeo vya wanaohusika badala ya jina lao “Daktari,muuguzi,mgonjwa”

(xi) Kudokeza mambo/kutokamilisha usemi “ni acute”

***Sifa nne za kwanza. Ataje sifa na mfano, bila mfano asipate alama”***

- c. (i) Huzungumzwa na watu wengi nchini.  
(ii) Hubeba amali, utamaduni na historia ya watu wengi nchini.  
(iii) Hukidhi mahitaji ya mawasiliano.  
(iv) Hutoa hisia za kikabila na kuwafanya watu kuhisi kuwa taifa moja.  
(v) Huwa imeidhinishwa na sheria za nchi husika.  
(vi) Huibua hisia uzalendo na fahari miongoni mwa wananchi.  
(vii) Huwa lugha ya kiasili au kienyeji.  
(viii) Huwapa watu utambulisho katika jumuiya ya kimataifa.

